

## Maswali

1. Mbona Ibrahimu hakutaka Isaka aoe mke anayeishi karibu?
2. Ibrahimu alitaka Isaka aoe mke wa namna gani?
3. Ibrahimu alituma nani kumtafutia Isaka mke?
4. Eliezeri alienda kutafutia Isaka mke wapi?
5. Eliezeri aliuliza Mungu ampe ishara gani?
6. Mwanamke aliyekuja kutoka mjini alifanya nini Eliezeri alipomuuliza ampe maji?
7. Yule mwanamke alitwa nani?
8. Eliezeri aliambia wazazi wa Rebeka nini?
9. Nani alisaidia Eliezeri kupata mke mzuri wa Isaka?
10. Mbona Ibrahimu alifurahi?

## Majibu

1. Wanawake walioishi karibu walikuwa waovu tena hawakupenda Mungu.
2. Ibrahimu alitaka Isaka aoe mke mzuri na anayependa Mungu.
3. Ibrahimu alituma Eliezeri amtafutie Isaka mke.
4. Eliezeri alienda Harani.
5. Eliezer aliuliza Mungu ishara kwamba mwanamke atakaye mpa maji anywe na anyweshwe ngamia ndiye.
6. Yule mwanamke alipea Eliezeri na ngamia maji wakanywa.
7. Yule mwanamke alitwa Rebeka.
8. Eliezeri aliwambia kwamba Rebeka ndiye mke halali wa Isaka.
9. Mungu alisaidia Eliezeri kupatia Isaka mke mzuri.
10. Ibrahimu alifurahi kwa sababu Isaka alipata mke anayependa Mungu.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 1 Mwaka wa 3



# 7 Mke kwa Isaka

## Marejeo

Mwanzo 24

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Ibrahimu alikuwa na hekima na akamtafutia Isaka mke anayependa Mungu. Mungu alisaidia kwa sababu Ibrahimu alimwamini.

## Maneno maalum

- 7.1 Isaka + mke + mwanamke anayependa Mungu + Eliezeri alisaidia + Harani + Mungu alisaidia
- 7.2 Eliezeri + Harani + kisima + wanawake wanakuja maji + omba + nyweshwa ngamia
- 7.3 Mwanamke mzuri + uliza maji + nyweshwa ngamia + Eliezeri alishukuru Mungu
- 7.4 Rebeka + mawe ya dhahabu + wazazi + Mungu alisaidia + mke sawa wa Isaka + kwaheri + kutana na Isaka
- 7.5 Isaka na Rebeka + oana + furahi + mke mzuri


**7.1** Ibrahimu alikuwa ni mzee na mwanawe Isaka alikuwa sasa mtu mzima. Ibrahimu alikuwa na hofu sana kwa sababu wakaazi wa pale walikuwa waovu. Hawakupenda Mungu. Ibrahimu hakupenda Isaka aoe mke asiyempenda Mungu. Aliamua kwamba lazima amtafutie Isaka aoe mke anayependa Mungu tena awe mkarimu na mzuri.

Eliezeri mtumishi wa Ibrahimu alimwaahidi kwamba atampatia Isaka mke mzuri. Ibrahimu aliuliza Mungu amsaidie. Ibrahimu aliambia Eliezeri aenda kwa mji wa Harani anakoishi nduguye.

Tukimfurahisha Mungu, yeye huwa tayari kutusaidia kila wakati. Ibrahimu alifurahisha Mungu kwa sababu aliamini Mungu kumtafutia Isaka mke mzuri. Kama Isaka angeoa mke muovu, yeye pia angekuwa muovu. Kwa hivyo Mungu alisaidia Ibrahimu kumpatia Isaka mke mwema, mzuri na mkarimu.

**7.2** Eliezeri alisafiri mwendo mrefu ili afike Harani. Alienda mpaka kwa kisima kando ya kuta za mji. Bunde tu wanawake watakuja kuteka maji kama kawaida yao kila jioni. Eliezeri aliambia Mungu, “Wanawake watakapokuja kutega maji nitawauliza wanipe maji ninywe. Kama kutakuwa na mmoja mzuri awe mke wa Isaka, tafadhali anipe mimi maji ninywe na hata anyweshe ngamia pia. Hii ndiyo itakuwa ishara kwamba yeye ndiye mke halali wa Isaka.”

**7.3** Papo hapo, mwanamke mzuri alitokea kutoka kwa milango za mji akija kuchota maji. Eliezeri alimwomba ampe maji ya kunywa. Alipomaliza kupea Eliezeri, alipea ngamia pia zikakunywa. Eliezeri alifurahi sana kwa sababu kwa kupea ngamia maji, Mungu alikuwa ameonyesha Ishara kwamba yeye ndiye mke mzuri wa Isaka. Eliezeri alishukuru Mungu kwa kumsaidia.



**7.4** Jina la mwanamke mzuri lilikuwa Rebeka. Alikuwa mpwa wa Ibrahimu. Eliezeri alipea Rebeka mawe ya dhahabu na vitu vingine vizuri kama zawadi kutoka kwa

Ibrahimu. Eliezeri alienda na Rebeka nyumbani kwao. Aliambia wazazi wa Rebeka kwamba amekuja Harani kutafutia Isaka mke mzuri. Aliwambia vile Mungu alikuwa amemwonyesha kwamba Rebeka ndiye mke halali wa Isaka. Walifurahi kusikia kwamba Rebeka atakuwa na mume mzuri vile.

Asubuhi na mapema, Rebeka aliwapa mama, baba na nduguye, “Heri njema.” Mara tu waliondoka kwenda safari ndefu na Eliezeri. Siku moja jioni, Isaka alikuwa anatembea uwandani. Akaangalia kwa umbali na kuona ngamia zinakuja, haraka haraka akaenda kukutana nao. Eliezeri alieleza Isaka vile kila kitu kilikuwa.

**7.5** Isaka alimpenda Rebeka sana. Rebeka naye alimpenda Isaka sana. Isaka na Rebeka walioana na wakaishi kwa furaha. Ibrahimu alifurahi kwa sababu Isaka alioa mke anayependa Mungu. Alishukuru Mungu kwa kumsaidia.